OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI KONDOA
JARIDA LA HALMASHAURI

Julai— Septemba2020

# Mhe. Waitara awaasa wanafunzi Shule ya Wasichana Kondoa



Naibu Waziri wa OR TAMISEMI Mhe.Mwita Waitara akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Msoleni Dakawa (wa kwanza kulia waliosimama), Mkuu wa Shule ya wasichana Kondoa Mwl. Frola Nussu pamoja na Wanafunzi wa shule hiyo alipotembelea shuleni hapo.

## SERA YA UHARIRI

Madhumuni ya Jarida hili ni kuhabarisha na kuelimisha wananchi juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Halmashauri ya Mji Kondoa. Aidha Sera, Mipango na utekelezaji wa miradi ya maendeleo inafafanuliwa kupitia jarida hili. Isipokuwa pale inapokatazwa habari za Jarida la Halmashauri ya Mji Kondoa zinaweza kunukuliwa ili mradi Mhariri ajulishwe kwa maandishi.

# NENO KUTOKA KWA MKURUGENZI



**Msoleni Dakawa**

**Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Kondoa**

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha hadi siku ya leo na kumaliza salama utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika kipindi cha robo ya kwanza (Julai—Septemba) kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Pili nawapongeza kwa dhati watumishi wa Idara ya Fedha wakiongozwa na Mkuu wa Idara CPA (T) Onesmo Mwonga kwa kujitolea kwa hali na mali na kuhakikisha wanakamilisha salama zoezi la ufungaji wa hesabu za mwisho lakini pia na wakuu wa Idara kwa ushirikiano wao waliounyesha katika kufanikisha kazi hiyo.

Tatu nazipongeza Idara za Kilimo na Mifugo katika kipindi hicho kwa ushiriki katika maonesho ya Wakulima na Wafugaji Nanenane mkoani Dodoma na kuibuka washindi wa kwanza kikanda kwa upande wa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na mfugaji kuzawadiwa kiasi cha shilingi milioni mbili.

Kipindi hicho pia Halmashauri ya Mji Kondoa ilianza kufanya kazi za uchaguzi mkuu kwa kuanza na zoezi la utoaji wa fomu za wagombea wa ubunge na udiwani hadi kuwapata wagombea ambao wanaendelea na kampeni na hadi mwezi Oktoba 2020 zoezi linaendelea vizuri tayari kwa upigaji kura tarehe 28/10/2020.

Aidha katika kipindi cha robo ya kwanza Julai hadi Septemba 2020 Halmashauri ya Mji imepokea fedha kiasi cha Shilingi 281,644,164.75 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (TASAF Tshs. 137,566,000, Elimu bila Malipo Tshs. 143,004,624.75 na mradi wa Malaria Tshs. 1,073,540) na kuifanya Halmashauri kupokea asilimia 5.6 ya bajeti ya miradi ya maendeleo.

Hata hivyo kwa kipindi cha Julai hadi Septemba Halmashauri kupitia mapato ya ndani imekusanya shilingi milioni 374,900,999.49 sawa na asilimia 27 ya lengo la makusanyo kwa mwaka 2020/2021 na kutoa shilingi milioni 33,141,000 ikiwa ni asilimia kumi ya makusanyo kwa ajili ya mikopo ya Vijana, Wanawake na watu wenye ulemavu

Mwisho niwaombe wananchi wa Halmashauri ya Mji Kondoa kujitokeza kwa wingi siku ya Jumatano ya tarehe 28/10/2020 ambayo ni siku ya Uchaguzi Mkuu kwa ajili ya kumchagua Rais, Mbunge na Diwani na kuwasihi kuepuka kujihusisha katika matukio ambayo yatapelekea uvunjifu wa amani na mara baada ya kupiga kura wananchi wanapaswa kurudi nyumbani kusubiri matokeo.

**Bodi ya Uhariri**

Msoleni Dakawa

Sekela Mwasubila

Leah Joseph

**Mawasiliano**

S.L.P 711 Kondoa

Simu: +255 712264912

Nukushi: +255262360313

**Mitandao ya Kijamii**

www: kondoatc.go.tz

Kondoa TC

kondoatc2015

KondoaTC

@KondoaTC

Barua Pepe
td@kondoatc.go.tz

# Mhe. Waitara awaasa wanafunzi Shule ya Wasichana Kondoa



**.Naibu Waziri wa OR TAMISEMI Mhe.Mwita Waitara akiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa Shule ya wasichana Kondoa pamoja na Wanafunzi wa shule hiyo alipotembelea shuleni hapo kukagua miradi ya Elimu.**

Naibu Waziri wa OR TAMISEMI Mhe. Mwita Waitara amewasihi wanafunzi wa Shule Sekondari ya Wasichana Kondoa kujifunga mikanda na kusoma kwa bidii ili wapate matokeo mazuri yatakayowawezesha kujiunga na vyuo vikuu watakavyo.

Ameyasema hayo alipokuwa anaongea na wanafunzi na walimu wa shule ya Sekondari ya Wasichana Kondoa baada ya kufanya ukaguzi wa majengo yaliyofanyiwa ukarabati mkubwa ikiwa ni moja ya shule zilizopata fedha za ukarabati wa shule

kongwe kutoka serikali kuu.

"Punguzeni usingizi wekeni ratiba ya kusoma ili mfaulu na nimepata taarifa zenu kuwa mnafanya vizuri nawapongeza bodi ya Shule, walimu na nyie wanafunzi kwa kuwa mnajisimamia vizuri na naamini kutoka hapo tutapata viongozi wazuri sana hapo baadae,"alisema Mhe. Mwita.

Aliongeza kuwa wanafunzi wametumwa elimu na si kubeba mimba kwa kuwa mtoto wa kike akisoma vizuri ana nafasi kubwa ya kuibadilisha familia na maisha yake kwa ujumla na muda wa wao kujipanga ni sasa ambapo wazazi wanawekeza kwao.

"Najua mmefurahia ukarabati uliofanyika kwa kuwa umeboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia pongezi nyingi kwa Mhe. Rais wetu kwa kuona umuhimu wa kukarabati shule hii hivyo tumwombee aendelee kuwepo ili maono yake ya awamu ya pili yatimie,"alisisitiza Mhe. Waitara

Aidha aliwashauri viongozi wa Wilaya kushirikiana na wadau wengine ili kuboresha na kuisogeza mbele elimu kwa kuwa kuna mambo ambayo yanafanywa na serikali na mengine yanapaswa kufanywa na wadau ambao wanapatikana ndani na nje ya wilaya.

Hata hivyo aliwapongeza viongozi kwa kusimamia vizuri fedha zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ukarabati kwa kuwa kwenye baadhi ya maeneo yaliyofanya vibaya viongozi wameishia kwenye vyombo vya sheria na kuwasisitiza kusimamia majukumu yao yote vizuri na kuwashukuru walimu kwa kufanya kazi kwa kujitolea.

Akiongea kwa niaba ya wanafunzi wenzake Rais wa Shule ya Wasichana Kondoa Getrude Gadau amesema shule yao ina changamoto ya upungufu wa maji, ukosefu wa gari la shule kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za shule na ubovu wa barabara ya kufika shuleni hapo.

Akijibu changamoto hizo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Msoleni Dakawa amesema kuwa changamoto ya barabara inaendelea kufanyiwa kazi kwa kuwa ipo katika miradi ya kimikakati na itawekewa lami na kuchimba kisima kirefu ambacho kitasaidia wanafunzi na wananchi wa jirani.

# SERIKALI KUENDELEA KUPAMBANA NA UNYANYASAJI DHIDI YA WAZEE



**Wazee wakiwa wanasikiliza hotuba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Idara kuu ya maendeleo ya Jamii Dkt John Jingu (pichani hayupo) wakati wa maadhimisho ya siku ya wazee katika viwanja vya sabasaba Kondoa Mjini**

Katika Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wazee Serikali imesema itaendelea kupambana na unyanyasaji wa Wazee nchini ikiwemo kudhibiti vitendo vya mauaji ya Wazee.

Hayo yamesemwa Wilayani Kondoa mkoani Dodoma na Katibu Mkuu Wizara ya Afya Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii Dkt. John Jingu wakati wa Maadhimisho ya Kimataifa Siku ya Wazee kwa Mkoa huo.

Aidha Dkt. Jingu ameongeza kuwa Serikali inafanya jitihada za kuwatunza Wazee hasa wasiojiweza kwa kuboresha makazi ya Wazee yanayosimamiwa na Serikali.

"Jamii tumewasikia Wazee wetu ni jukumu letu kuwalinda wazee hawa wafurahie maisha na ni wajibu wetu tusiukimbie".

"Hawa wazee nao wakati wanatulea wangesema hawana muda na sisi tungekuwa wapi tungekuwa wakina nani tuwatunze wazee wetu" alisema Dkt. John Jingu

Akitoa taarifa ya maboresho ya huduma za Wazee kwa ngazi ya Wizara Kamishna wa Ustawi wa Jamii Dkt. Naftali Ng'ondi amesema Serikali imeendelea kuwatunza wazee wasiojiweza katika Makazi 13 yanayosimamiwa na Wizara kwa kuwapatia huduma stahiki kwao.

"Tunahudumia wazee 281 mpaka sasa katika Makao haya tunayoyahudumia kwa kuwapatia wazee huduma za Afya na huduma nyingine muhimu" alisema.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Maduka Kessy amesema kuwa Mkoa wa Dodoma umeendelea na jitihada za kuwatunza Wazee kwa kuboresha huduma mbalimbali zikiwemo huduma za Afya na kuwaasa Jamii kuwajibika kuwatunza.

"Sisi tunaongoza kwa asilimia 25 ya kuwawezesha wazee kujiunga na huduma za Afya kwa kujiunga katika Bima ya Afya iliyoboreshwa ili kuwawezesha kupata huduma Bora" alisema

**"WAZEE NI HAZINA TUWATUNZE"**

# NMB KONDOA WAZINDUA WIKI YA HUDUMA KWA MTEJA NA WATUMISHI KONDOA MJI

Benki ya NMB Kondoa wameanza maadhimisho ya wiki ya huduma kwa mteja kwa kukutana na kuongea na kula keki kwa pamoja na watumishi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Makao Makuu.

Maadhimisho hayo yamefanyika katika ukumbi wa Kituo cha Uwekezaji Kondoa ambapo yalihudhuriwa na watumishi wa Makao Makuu na watumishi wa Benki ya NMB Kondoa wakiambatana na Meneja wa benki hiyo.

Akiongea awali Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Msoleni Dakawa amewapongeza watumishi wa benki hiyo kutokana na huduma wanayotoa kwa watumishi kwa kipindi chote wanachofanya kazi na Halmashauri ya Mji na kuahidi kuendelea kuwaamini ili kufikia malengo.

"Tunashukuru kwa kutukumbuka leo kweli tumekuwa pamoja tunaalikana katika matukio mbalimbali na toka muanze kutuhudumia hamjawahi kutuangusha tunawashukuru sana", amesema Mkurugenzi Dakawa.

Kwa upande wake Meneja wa NMB Kondoa Francis Malire amesema kuwa watoa huduma wameamua kutenga wiki ya huduma kwa wateja ili kujirekebisha pale wanapofanya vibaya. "Nguo hata kama ikiwa safi bado inaweza kuwa na uchafu lakini hata tukijiuliza taulo linachafukaje ikiwa tunalitumia tukiwa wasafi? Basi hata sisi inawezekana tunafanya vizuri lakini kuna sehemu tunajisahau na ndio maana tunaweka wiki hili la hudumakwa mteja ili tuwe karibu na wateja",amesema Malire.

Hata hivyo kwa upande wao wameanza kuadhimisha wiki hiyo kwa kuzindua huduma kwa wateja mpya tatu ambapo mteja atawasiliana moja kwa moja na benki kidigitali.

"Tunazindua huduma za kidijitali zaidi ambapo kuanzia sasa mteja atauliza swali au huduma yoyote kwa WhatsApp namba 0747333444, pia tumezindua huduma ya kupata mrejesho kwa kutumia simu janja ambapo mteja ataipakua kwenye simu yake na kuitumia katika ATM mashine na kupata majibu hapohapo na huduma ya mwisho ni mteja mbaye atanunua luku bila kupata token atapiga simu huduma kwa mteja 0800002002 na kisha kutajiwa token za kuingiza,"amesema Malire.



Mkurugenzi Msoleni Dakawa pamoja na Afisa Utumishi Lucy Timba wakikata keki wakati wa maadhimisho ya wiki la huduma kwa mteja yalna Benki ya NMB tukio hilo limejjiri katika ukumbi wa Kituo cha Uwekezaji Kondoa

**MAHUSIANO MAZURI YA TAASISI NI MAENDELEO YA TAASISI ZOTE MBILI NA ENEO HUSIKA**

# WENYEVITI NA WATENDAJI WA MTAA,WALIMU WAKUU WATAKIWA KUWAJIBIKA

Wenyeviti na Watendaji wa mitaa, Walimu wakuu, Wajumbe wa Kamati za shule na wajumbe wa Kamati za ujenzi za shule wametakiwa kuwajibika na kuwa waadilifu ili kutimiza malengo yaliyowekwa na Serikali katika maeneo yao.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Msoleni Dakawa alipofanya vikao na viongozi hao katika Shule za Msingi Maji ya Shamba na Bolisa.

"Nasikitishwa sana na hali ya ujenzi katika shule zenu mpo nyuma sana na muda unakimbia fedha zipo kwenye akaunti zenu kwa zaidi ya mwezi sasa ujenzi hauendelei mnakwama wapi katika kusimamia ujenzi? Aliuliza Mkurugenzi Dakawa.

Ameongeza kusema kuwa kunabaadhi ya walimu wakuu wamekosa uzalendo kwa kuongea na mafundi (Local Fundi) ili wapatiwe fedha ndiyo wawapatie kazi katika ujenzi unaoendelea baada ya kupata fedha za EP4R hali inayosababisha miradi kuchelewa kukamilika na kuwanyima haki ya msingi wanafunzi.

"Uongozi wa Kata na mitaa ndiyo wasimamizi wa miradi ya maemdeleo katika maeneo yenu lakini mnakaa pembeni sivo sawa na

Mtaa, tuwahamasishe wananchi wajitolee nguvu kazi ili fedha itakayobaki tuboreshe miundombinu mingine ya shule ikiwemo kununua madawati, viti na meza za walimu, vyoo vya



Mkurugenzi Msoleni Dakawa (aliyesimama) katika kikao na wajumbe wa kamati ya Ujenzi, walimu, na wajumbe wa serikali ya Mtaa wa Bolisa(Hawapo pichani)

walimu ",amesisitiza Mkurugenzi Dakawa.

Hata hivyo amewataka viongozi hao kuwa na uchungu na mali za shule kwani kinyume na hapo ni sawa na kutowatendea haki wananchi wanaowaongoza na kuwaagiza kukamilisha miradi hiyo ndani ya mwezi huu.

Halmashauri ya Mji Kondoa imepokea zaidi ya shilingi milioni 291 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, vyoo na umaliziaji wa nyumba za walimu katika shule za Msingi Mongoroma, Kingale, Mpalangwi, Iboni, Maji ya Shamba, Miningani na Shule ya Sekondari Ula.




Wajumbe wa kamati ya ujenzi wa shule, walimu.watendaji wa mitaa na kamati ya serikali ya mtaa wa Bolisa wakimsikiliza Mkurugenzi watati wa kikao cha mikakati ya kumaliziaji wa madarasa katika Shule ya Msingi Bolisa

# "Mikopo itumike ilivyopangwa kwenye maandiko ya miradi"- Mkurugenzi Dakawa

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Msoleni Dakawa ameviasa vikundi vilivyopata mikopo iliyotokana na asilimia 10% ya mapato ya ndani kutumia kwa kufuata maandiko ya miradi waliyoandika wakati wa kuomba mikopo hiyo.

Kauli hiyo ameitoa wakati wa hafla fupi ya kukabidhi hundi yenye thamani ya shilingi milioni 39.5 iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa robo ya tatu iliyofanyika katika jengo la kituo cha uwekezaji kilichopo Kondoa Mjini.




Mkurugenzi Msoleni Dakawa akikabidhi hundi yenye thamani ya shilingi milioni 39.5 iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake,vijana na watu wenye ulemavu ikiwa ni sehemu ya asilimia 10 ya mapato ya Halmashauri.

"Tunataka mkakue kibiashara na kufungua makampuni yatakayowapa fursa ya kufanya biashara popote ndani na nje ya nchi na kupata mikopo mikubwa zaidi ambayo itawaongezea uzalishaji na kukuzakipato chenu,"alisema Mkurugenzi Dakawa.

Aidha aliwashauri kuiga mfano wa vikundi vya watu wenye ulemavu waliopewa mkopo na kumaliza marejesho yao yote ambapo kwa kufanya hivyo wanatoa fursa kwa wengine kupata mikopo hiyo.

"Nasisitiza tuidhibiti mianya ya rushwa katika kupata mikopo hii kwa kuwa sisi sote ndio ambao tunapaswa kuijenga Kondoa ili kupata maendeleo na vyote vinawezekana tukiwa na amani na upendo miongoni mwetu," alisisitiza Mkurugenzi Dakawa.

Awali akisoma taarifa ya utoaji wa Mikopo Afisa Maendeleo ya Jamii Irene Mosha amesema kuwa hadi kufikia sasa Halmashauri imetoa mikopo ya asilimia kumi ya mapato ya ndani yenye jumla ya shilingi milioni 196 kwa vikundi 55 na imekusanya kiasi cha zaidi ya milioni 80 ikiwa ni marejesho kutoka kwa vikundi hivyo.

Kwa upande wake Meneja wa Benki ya NMB Kondoa Francis Malile alipongeza uongozi wa Halmashauri kwa kuongeza ukusanyaji wa mapato ambayo yanarudi kwa jamii kwa njia ya mikopo inayotolewa.

"Nawashauri mkatumie vizuri fedha hizi na hizi ni kianzio tu mmepewa mkakuze mitaji yenu ili Kondoa iendelee na kwa sasa tumeanzisha akaunti ya PAMOJA kwa ajili ya vikundi na haina makato yeyote tuitumie," alisema Meneja Malile.

Halmashauri imetoa hundi yenye thamani ya shilingi milioni 39.5 ikiwa ni mikopo kwa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2019/2020 na imehudhuriwa na wakuu wa Idara, Meneja wa Benki ya NMB na wawakilishi wa vikundi vilivyopatiwa mikopo hiyo.




Kikundi cha watu wenye ulemavu wakipewa hundi ya mfano na Mkurugenzi

# Wanawake Kondoa Mji Washauriwa kudumisha Upendo na Mshikamano.



**Mkurugenzi Msoleni Dakawa akitoa hotuba katika kongamano la wanawake lililofanyika katika ukumbi wa CCM Kondoa hivi karibuni.**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Msoleni Dakawa amewaasa wanawake wa Halmashauri hiyo kudumisha upendo, amani na mshikamano ili kuweza kufanikiwa katika shuguli zao za kuwaletea maendeleo.

Kauli hiyo ameitoa wakati wa Kongamano la wanawake wa Halmashauri ya Mji Kondoa lililofanyika katika ukumbi wa CCM hivi karibuni.

"Kinamama wa Kondoa kwa ujumla wenu inabidi mpendane, mshirikiane na msaidiane ili kuweza kupata maendeleo, kwani mshikamano huleta nguvu na sehemu yeyote ile ili iendelee kwa haraka basi nafasi hiyo apewe mwanamke," amesema Dakawa.

Aidha Mkurugenzi Dakawa amesema katika kila familia yenye maadili na nidhamu mwanamke amehusika kwa kiasi kikubwa katika kutoa mchango wake licha ya wao kujiona ni watu wa kawaida lakini ukweli utabakia kuwa wanawake ni jeshi kubwa.

"Tumeona jinsi Halmashauri ya Mji Kondoa imeweza kuwanyanyua akina mama ili waweze kujikwamua kimaisha kwa kutoa mikopo ya wanawake japokuwa taratibu na hatuwezi kuwafikia wote kwa wakati mmoja, lakini vikundi vyenye sifa ya kupata mkopo vitapata kwa wakati ili mwisho wa siku vikue na kuwa kampuni na kuweza kutoa ajira kwa watu wengine hatimaye kukuza uchumi wao, Halmashauri yetu na taifa kwa ujumla," amesisitiza Dakawa.

"Natamani shughuli za uchaguzi zikiisha basi tufanye kongamano kubwa litakalohusisha wanawake,wanaume navijana ambapo tutaita watu walio

fanikiwa kiuchumi na wametokea Kondoa watuhamasishe ni kwa namna gani walifikia pale walipo," ameongeza Dakawa.

Hata hivyo Mkurugenzi Dakawa aliwatakia ushindi wagombea wa nafasi mbalimbali za kisiasa ili mwisho wa siku waungane katika shuguli za ujenzi wa taifa na kuwaomba wananchi wote kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi ili wachague viongozi bora kwa maendeleo ya wanakondoa.

Kwa upande wake Afisa Maendeleo ya Jamii Bi. Irine Mosha ametoa taarifa fupi ya Idara ya Maendeleo ya Jamii ambapo amesema wameweza kutoa mkopo wa shilingi milioni 196.6 kwa ajili ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na bado wataendelea kuwa na makongamano na midahalo na kuomba kila mtu kwa nafasi yake aliyonayo kuendelea kuhamasisha jamii ili watu waweze kujitokeza kwenye midahalo itakayojitokeza kwani huo ni mwanzo tu.

Kongamano la wanawake wa Mjini Kondoa limefanyika ili kuweza kujadili na kutambua fursa mbalimbali zinazoweza kumkwamua mwanamke kiuchumi na kubeba kauli mbiu ya "Mwanamke , Upendo na Amani", kongamano hili limeenda sambamba na maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya mtoto wa kike,ambapo mgeni rasmi alikuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji

# MATUKIO MBALIMBALI KUANZIA MWEZI AGOSTI-OCTOBER 2020




**Wanafunzi wa shule ya wasichana Kondoa wakifanya onesho la sarakasi katika siku ya kumuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere**



Wawakilishi kutoka benki ya NMB na CRDB, Dawati la jinsia pamoja na wanafunzi wa shule na vyuo ni baadhi ya washiriki waliohudhuria kongamano la wanawake



Mkurugenzi Dakawa akiwa katika kikao pamoja na watendaji wa mitaa, wakuu wa shule na wajumbe wa kamati za shule na ujenzi



**Wanachuo cha Ualimu Bustani wakipokea zawadi kutoka kwa wadau wa elimu ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya mtoto wa kike duniani**



**Mkurugenzi Msoleni Dakawa akiwa pamoja na watumishi wa Halmashauri ya Mji Kondoa wakati wa hafla fupi ya kuwapongeza kwa ukusanyaji mzuri wa mapato. .**



**Mmoja wa wanufaika wa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya wanawake,vijana na watu wenye ulemavu.**